

Haki za Wahamiaji wafanyakazi wa Ngonu

Makala ya Uhawilishaji Maarifa

yaliyo fadhiliwa na Chuo Kikuu cha Kichina cha Hong Kong

Makala hii ni muhtasari ulioandaliwa kwa ajili ya kutoa rejea ya haraka. Kwa habari zaidi juu ya mada zote zilizotajwa hapa, rejea zinaweza kufanywa kwa mmojawapo wa watoa msaada walioorodheshwa nyuma au kwa makala nzima pamoja na rejea zake zote yaweza kupatikana kwa anuani ya mtandao wa Chuo Kikuu cha Kichina cha Hong Kong (CUHK).

Marejeo yote kwa watoahuduma ndani ya makala hii yanaongozwa na jedwari linaloainisha anwani kamili, undani wa huduma inayotolewa, na lugha zinazotumika vimeainishwa mwishoni mwa makala hii.

Sehemu I

Jinai na maana ya huduma zinazotolewa na wafanyabiashara ya ngono

Je ni halali kuwa mfanyakazi wa ngono Hong Kong?

Ukahaba ni halali katika Hong Kong, lakini karibia kila kitu kihusianacho na ukahaba siyo halali. Mtu anaweza kutozwa faini ya hadi \$10,000 au kufungwa jela hadi miaka 10 (ingawa miezi 2 ni ya kkiwango cha mwenendo wa kesi), kulingana na kosa.

Nikinyume cha sheria:

1. Kufanya “tendo kinyume na maadili” ikiwa ni pamoja na
 - Kuanzisha mazungumzo na mteja au kutumia lugha ya mwili, kujieleza au mavazizi ya kuashiria uwepo wako kwa wateja
 - kutaja huduma zilizopo na bei
 - kufanya huduma ya ngono kwa ajili ya maslahi ya kibiashara.
2. Kupangisha, kusimamia au kusaidia katika usimamizi wa kuanzishwa kwa madhumuni ya ukahaba, au kazi kuanzishwa massage bila leseni.
3. Kutunza, kupangisha, kusimamia au kusaidia katika kuanzishwa kwa madhumuni ya ukahaba, au kuendesha uendeshaji wa maseji bila leseni.
4. Wakitambua kuwa wanaishi kwa mapato ya wengine kwa kutumia njia ya ukahaba ikiwa ni pamoja na biashara ya binadamu kwa ajili hiyo.
5. Kutangaza huduma za ukahaba.
6. Kwa wamiliki wa viza mbili za kuingilia (double entry visas), visa za utalii, visa za kibiashara au kwa lengo la kuwatembelea jamaa zao kushiriki katika shughuli yeyote kwa ajili ya fidia ya kifedha (ikiwa ni pamoja na ngono) au kuzidisha muda wa kuishi baada ya visa kwisha (adhabu mbalimbali zitaanzia faini ya \$50,000 to \$600,000 na hadi kifungo cha miaka 14 jela kwa kutumia nyaraka za kugushi).

Siyo kinyume cha sheria kumjibu mteja aliyeanzisha mazungumzo, kufanya matendo ya ngono katika majengo ya binafsi kwa watu wenye umri wa miaka 18 au zaidi na kusimama mitaani.

Kumbuka: wafanyakazi ya ngono wanatakiwa kubeba uthibitisho wa utambulisho wao (kama kila mmoja anamiaka 15 na zaidi) katika mfumo wa nyaraka halali za kusafiria, kama vile kitambulisho cha uraia wa Hong Kong, nyaraka au barua zinazotambulika kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa la Wakimbizi (UNHCR) kwa wakimbizi na wanaotafuta hifadhi au pasipoti (hati ya kusafiria). Mtu yeyote ambaye atashindwa kutoa uthibitisho wa utambulisho anaweza kukamatwa, kuhojiwa na kutozwa faini. Kukamatwa na kuwekwa kizuizini

Mamlaka ya kisheria inaouwezo wa kumsimamisha mtu yeyote na kumtaka kuthibitisha utambulisho wake, kama mtu huyo atakuwa anafanya matendo ya kutiliwa mashaka, mtu huyo azuiliwe endapo kunashaka kuwa kutenda kosa na mpekue kama anasilaha. Kama ukamataji utafanyika, basi afisa mkamataji lazima amueleze mtu huyo sababu za kukamatwa kwake.

Polisi wenyekibali, wanaweza kuingia na kufanya upekuzi kwenye majengo kama kuna ushahidi wa kutosha kushakia kuwa kosa limetendeka au lilitendeka kwenye majengo hayo. Aidha, kamishina wa polisi anaweza kuidhinisha polisi kuingia kwenye majengo bila taarifa kuhoji mtu yeyote ndani yake kuangalia kama kuna wasichana wowote wamepotea au kama kuna wasicha wowote chini ya umri wa miaka 16 wanafanya kazi ndani ya majengo hayo.

Mtu anaweza kuwekwa kizuizini baada ya kukamatwa. Mara baada ya uchunguzi, kama kuna ushahidi wa kutosha, mtu huyo atashitakiwa, na aidha (i) ataachiliwa kwa dhamana ilibaadaye ahudhulie mahakamani au (ii) atawekwa kizuizini na baadaye kufikishwa mbele ya hakim, kwa kawaida ndani ya masaa 48 isipokuwa kama ameondolewa au kufukuzwa nchini chini ya sheria za uhamiaji. Kwaujumla, mtu ataachiliwa kwa dhamana endapo atabainisha kiwango cha kuridhisha au kwa dhamana ya kiasi fulani cha fedha kilichotajwa, haraka iwezekanavyo, isipokuwa kama kosa kwa asili yake ni kubwa au inaonekana kwamba mtu huyo anapaswa kuwekwa kizuizini kwa minajili ya kufikishwa mbele ya hakim. Wafanyakazi wahamiaji wa ngono wasio na kitambulisho cha uraia wa Hong Kong hawawezi kuachiliwa moja kwa moja kwa dhamana ingawa hawazuiliwi kuomba dhamana kupitia mwanasheria kwenda kwa jaji au mahakama kuu.

Kuwekwa kizuizini pia kumehalalishwa kwa ajili ya kufanya uchunguzi wa hadhi ya uhamiaji:

1. hadi siku 7 kama mtu anashakiwa kukiuka sheria ya uhamiaji
2. hadi masaa 48 kama mtu atashakiwa kuingia katika Hong Kong bila idhini sahihi, akisubiri uamuzi wa kukubaliwa au kukataliwa ruhusa ya kuingia nchini.
3. hadi siku 28 kama kutakuwa na sababu za msingi za kumshakia mtu kama kafukuzwa kwasababu amepatikana na hatia katika Hong Kong kwa kosa liwezalo kumpeleka jela kwa muda usiopungua miaka 2, na/au vyovyote vile gavana atakavyoona inafaa kwa manufaa ya jamii.
4. Kwa muda usiojulikana, kutegemea na kuondolewa au kufukuzwa kwa mtu. Na kama kuondolewa kutaamriwa mtu huyo anaweza kukata rufaa ndani ya masaa 24 na hawezi kuondolewa ndani ya muda wa kukata rufaa.
5. Wafanyabiashara ya ngono wanaweza kuwekwa kizuizini hadi siku 5 kama polisi watahitaji muda zaidi kufanya uchunguzi na kukusanya ushahidi.

Haki za watu wakati wa kushughulika na polisi au huduma za uhamiaji

1. Mtu yeyote aliyekamatwa atapewa taarifa wakati wa kukamatwa juu ya sababu za kukamatwa, na atajulishwa mara moja taarifa ya mashitaka yeyote yanayo mkabiri, atafikishwa mara moja mbele ya hakim na ni haki kusikilizwa ndani ya muda wa kuridhisha. Waathirika wa kukamatwa au kuwekwa kizuizini kinyume cha sheria wanahaki ya kisheria ya kupata fidia.
2. Watu wanaweza kuomba na kuchukua kumbukumbu za utambulisho wa afisa wa polisi.
3. Watu wanahakii ya kukataa kutoa taarifa kama zile za binafsi na familia, wanahaki ya kukataa kutia sahihi hati yeyote, kukataa kuchukuliwa picha zao wenyewe au majengo yao.
4. Upekuzi wa maungo ya mwili lazima ufanywe na afisa wa jinsia moja, kuwe na kibali, lazima ufanywe mbele ya maafisa wa jinsia moja sawa na mtu mwenyewe katika faragha ya kutosha.
5. Wakati wa shughuli maalum, maafisa wa polisi wanaruhusiwa kulipia huduma ya ngono itakayoisha muda mufupi baada ya tendo kamili la ashilio la ngono, maafisa hatakiwi kuuliza bei au asili ya huduma zinazotolewa, hapaswi kuanzisha mgusano wa mwili na mfanyabiashara ya ngono, hatakiwi kukubali huduma ya ngono (ingawa hii haijumuishi kukubali huduma ya punyeto) na hapaswi kupokea fedha.
6. Afisa mkamataji lazima aeleze sababu ya ukamataji na kutoa Maelezo ya Onyo (haki ya kukaa kimya).

7. Mtu akiwa kizuizini anaweza kuomba msaada wa kisheria kwa kupiga simu binafsi au kuwasiliana kwa maandishi; kuwa na mwanasheria au wakili wakati wa mahojano yeyote; kufanya mawasiliano ya binafsi au kukataa mawasiliano na mwanasheria au wakili kwa madai kuwa wamekuwa na mawasiliano na mtu wa tatu kwaniaba ya mtuhumiwa; kuomba orodha ya wanasheria iliyochapishwa na shirika la sheria la Hong Kong; kuiomba polisi iwajulishe rafiki au ndugu uwepo wao katika kituo cha polisi ili waweze kuwasiliana na ofisi za ubalozi husika. Aidha, mtu anayo fursa ya kuwasiliana na ndugu au rafiki kwa njia ya simu; anaweza kutembelewa na rafiki au ndugu kwa idhini ya afisa msaidizi; kuomba kupewa vifaa vya kuandikia; kuomba dhamana; kuomba huduma ya kutafisiriwa (ukalimani) na kupatiwa milo mitatu kwa siku ikiambatana na maji na huduma za afya ikibidi.

Kufanya malalamiko dhidi ya polisi kwa ukiukwaji wa maadili au kuomba msaada mahala ambapo haki imekiukwa

- Lalamika kwa afisa msaidizi wa kituo cha polisi.
- Piga simu namba 999.
- Piga simu kwa Zi Teng namba: +852 2332 7182 (simu ya msaada wa sheria kwa masaa 24).
- Piga simu kwa Malalamiko na Tawi la Upelelezi wa Nani (CIIB) namba: +852 2866 7700.
- Piga simu kwa Tume Inayojitegemea ya Kupambana na Rushwa namba: +852 2526 6366.

Sehemu II

Haki ya kisheria ya kuishi katika Hong Kong

Haki ya kisheria ya kuishi katika Hong Kong

Kila mtu anahitaji kuwa na visa/kibali cha kufanya kazi, kusoma, kuanzisha au kujiunga katika biashara yeyote au kuchukua ukazi au kubaki katika Hong Kong kama mgeni kwa muda mrefu zaidi kuliko muda ulioruhusiwa wa kuishi bila visa isipokuwa kama wanahaki ya kuishi au kuingia Hong Kong.

- Kwa taarifa zaidi – Haki ya sehemu ya makaazi ya uhamiaji
 - Kwamaulizo simu namba: +852 2824 6111.
 - Barua pepe: enquiry@immd.gov.hk
 - Tovuti: <http://www.gov.hk/en/residents/immigration/idcard/roa/eligible/>
- Taarifa zaidi juu ya kupata kitambulisho cha Hong Kong (vinatakiwa na watu wote wenye haki ya kuwa katika Hong Kong, ndani ya siku 30 tangu wawasili)
 - Simu ya kuomba nafasi ya huduma: +852 2598 0888 (24 hours).
 - Barua pepe: enquiry@immd.gov.hk
- Kuvunja masharti ya kuishi Hong Kong humsababishia mtu kupewa adhabu ikiwa ni pamoja na faini na kifungo, habari zaidi juu ya masharti ya kuishi Hong Kong yanaweza patikana katika tovuti hii: www.immd.gov.hk

Wakimbizi, wanaotafuta hifadhi, na watoamadai kwamujibu wa mkataba dhidi ya mateso (CAT)

Hong Kong haijaridhia mkataba wawakimbizi na kwahiyo haipokei wakimbizi. Watu wanaotaka kuwa na hadhi ya ukimbizi wanapaswa kuwasiliana na wakara wa wakimbizi wa umoja wa mataifa (UNHCR) ilikuanza kuchunguza hadhi ya ukimbizi wao, na kama wakifanikiwa wataweza kuhifadhiwa nchini Marekani au Kanada (lakini siyo katika Hong Kong). Wakati wa usajiri, mtu atawekwa kizuizini ilikuchunguza utambulisho na madhara ya kiusalama dhidi yake kabla hajapewa barua ya kutambuliwa (inayompa uhuru wa kutembea ndani ya nchi husika, ingawa hawatakuwa na haki ya moja kwa moja iliyo sawa na wale walioruhusiwa kuishi Hong Kong kisheria). Wakalimani watakakuwepo kuwasaidia waombaji katika mchatato wote, unaoweza kuchukuwa miaka mingi, na kwamba mtu anapaswa kusubilia na katika kipindi hicho haruhusiwi kuajiriwa Hong Kong. Kama mtu atakataliwa ombi lake la hadhi ya kuwa Mkimbizi, muombaji atarudishwa katika nchi yake ya asili (endapo mchakato wote wa rufaa/maombi ukishindikana; kwa taarifa zaidi juu ya utoaji maombi piga simu namba: +852 2294 2981). Vile vile kama mtu anatamani kutoa maombi ya ukimbi kwa misingi ya kwamba alikuwa akiteshwa/atateswa katika nchi yake ya asili, maombi hayo yatawasilishwa kwa mkurugenzi wa uhamiaji na yatashghulikiwa na kitengo kinachofanya

tathimini ya uteswaji kwa wahamiaji cha idara ya uhamiaji. Tangu mwaka 2008, ni ombi moja tu liliwahi kuzingatiwa/kukubaliwa hapa Hong Kong. Kwa maelezo zaidi waweza kuwasiliana na:

- Kitengo kinachohusika na utekelezaji na tathimini ya madai ya uteswaji kwa simu namba: +852 2829 3838
- Idara ya uhamiaji, simu namba: +852 2824 6111
- Barua pepe: enquiry@immd.gov.hk

Ukweli ni kwamba mtu kuwa mkimbizi, muomba hifadhi, au mtoa madai kwamujibu wa mkataba dhidi ya mateso haipelekei mtu huyo kushitakiwa au kuwekwa kizuizini katika Hong Kong. Kwa mujibu wa sheria za Hong Kong, hatua ya utekelezaji wa sheria ya kushitakiwa au kuwekwa kizuizini itachukuliwa endapo mtu huyo akikiuka sheria za Hong Kong kama vile kuajiriwa kinyume cha sheria au kuishi zaidi ya muda stahiki wa visa yake.

Kuongeza muda wa viza na uhamiaji

Taarifa juu ya namna ya kuongeza muda wa viza (siku 7 kabla ya ukomo wa viza za wageni na wiki 4 kwa wakaazi wasio wa kudumu bila kujumuisha wasaidizi wa majumbani) zinapatikana kwa:

- Simu namba: +852 2824 6111
- Barua pepe: enquiry@immd.gov.hk

Kwa wasaidizi wa ndani ni lazima kuomba kuongeza muda wa viza wiki 8 kabla ya ukomo wa viza ya muombaji. Maombi hayo yanaweza kufanywa kwa njia ya mtandao kupitia tovuti hii: www.gov.hk/esapplication.

Uhamiaji wa wanafamilia tegemezi

Mke, watoto ambao hawajaoa au kuolewa walio chini ya umri wa miaka 18 na wazazi wenye umri zaidi ya miaka 60 wa mtu ambaye ni mkazi wa kudumu wa Hong Kong au makazi mwenye muda maalumu wa kuishi Hong Kong (yaani, mkazi mwenye haki ya kuingia au mwenye kuruhusiwa kuishi bila masharti Hong Kong) wanaweza kuomba ruhusa ya kuishi naye. Vile vile wanafamilia hawa wanaweza omba ruhusa ya kuishi na mtu aliyeruhusiwa kuishi Hong Kong kwa ajili ya kuajiriwa au kwa ajili ya masomo au kwa ajili ya biashara au mkazi chini ya mpango bora wa udahili wa wakazi ukiondoa wakazi wa china-bara (isipokuwa kwa baadhi ya mazingira). Halikadhalika, itakuwa kwa wakaazi wenye asili ya kichina wanaoishi kwenye mkoa maalumu wa kiutawala wa Macau waliopata uraia wa macau kwa taratibu mbalimbali tofauti na utaratibu wa njia ya moja kwa moja ya mpango wa kibali cha makazi; na raia wa Afghanistan, Albania, Cuba and jamuhuri ya kidemocrasia ya watu wa Korea. Kutokana na ukosefu wa mipango rasmi kuhusiana na wadai wa hadhi ya ukimbizi, hifadhi, au wadai kwa mujibu wa mkataba dhidi ya mateso (CAT); hakuna sera zinazohusiana na wategemezi wa watu hawa ingawa watoto walio chini ya miaka 18 watafuata utaratibu wa maombi ule ule na kwamba familia itafikiriwa kwa ujumla wake.

Sehemu ya III

Huduma za afya

Huduma za afya kwa ujumla

Huduma za afya katika Hong Kong hutolewa na serikali na watu binafsi:

- Maeneo na maelezo ya mawasiliano ya huduma ya afya kwa umma yanaweza patikana katika tovuti hii: http://www.ha.org.hk/visitor/ha_visitor_index.asp?Content_ID=10084&Lang=ENG&Dimension=100&Parent_ID=10042
- Kuna hospitali za serikali 16 zikiwa na huduma za mambo ya ajali na ya dharura ambazo hutoa ushauri na tiba kwa wagonjwa wanaohitaji huduma ya dharura. Orodha ya idara zote za ajali na dharura zinapatikana kupitia tovuti hii: http://www.ha.org.hk/visitor/ha_visitor_index.asp?Content_ID=200246&lang=ENG
- Orodha ya hospitali za binafsi zilizosajiliwa zinapatikana katika tovuti hii: http://www.dh.gov.hk/english/main/main_orhi/list_ph.html

Huduma ya afya iliyopunguzwa bei (ruzuku ya serikali katika hospitali za umma), hutolewa kwa wenye vitambulisho vya uraia wa Hong Kong, watoto chini ya umri miaka 11 ambao ni wakazi wa Hong Kong na watu wengine walioidhinishwa na Mkurugenzi wa Afya. Kwa wamiliki wa vitambulisho vya uraia wa Hong Kong ambao hawana uwezo wa kugharimia ruzuku ya huduma za afya, zipo chaguzi zifuatazo:

- kwa watu wanaopata msaada kamili wa hifadhi ya jamii (CSSA) hawapaswi kulipia gharama za huduma za afya ya umma (siyo kwa wahamiaji haramu, ikiwa ni pamoja na wakimbizi, wanaotafuta hifadhi na watoa madai kwa mujibu wa mkataba wa mateso (CAT) amabo wamepitiliza muda wa ukomo wa viza zao).
- kwa makundi ya watu wanao ishi katika mazingira magumu katika jamii ambao hawapati msaada kamili wa hifadh ya jamii – CSSA (wagonjwa wenye kipato cha chini, watu wenye magonjwa sugu na wazee) , kuna msamaha wa matibabu anaostahili mtu kupata baada ya kuomba kupatiwa huduma za afya bure. Waweza tizama pia katika tovuti zifuatazo:
 - <http://www.ha.org.hk/haho/ho/hacp/122630e.htm>.
 - anuani na nambali za simu za kitengo cha tiba na huduma za jamii cha SWD http://www.swd.gov.hk/doc/rehab/MSSU-SWD_Eng_042011.pdf.
 - anuani na nambali za simu za kitengo cha tiba na huduma za jamii kilicho chini ya mamlaka ya hospitali http://www.swd.gov.hk/en/index/site_pubsvc/page_medical/sub_medicalsoc/.

Wakimbizi, watafutahifadhi, na watoa madai kwa mujibu wa mkataba wa mateso (CAT) wanaweza kutibiwa katika hospitali za serikali zitoazo huduma za tiba ya ajali na dharura kwa kibali kinachotambulika na wanaweza kuomba msamaha wa matibabu kupitia ofisi za idara ya ustawi wa jamii (SWD) ya hospitali. Watoa huduma mbalimbali hutoa msaada kwa wakimbizi na waomba hifadhi ikiwa ni pamoja na maono kwanza (Vision First), mpango wa ASTC unaoendeshwa na ISS, jumba la Chungking la matendo ya kikristo litoalo huduma kwa wakimbizi na waomba hifadhi (Christian Action Chungking Mansion Service for Refugees and Asylum seekers) ambapo mashirika kama vile UNHCR na HKRAC huwasaidia watu katika kupata matibabu maalumu kama hakuna msaada wa umma unaoweza kupatikana.

Huduma za afya ya akili na huduma kwa waathirika wa unyanyasaji wa kijinsia

Neno huduma ya afya ya akili linaelezea huduma zinazohusisha huduma mbalimbali za maswala ya afya ya akili ikiwa ni pamoja na ushauri nasaha, tiba ya kisaikorojia, msaada wa kisaikolojia na kijamii, na matibabu ya magonjwa ya akili, na huduma zinginezo. Kwa asili huduma zinazotolewa hutofautiana kwa kiasi kikubwa baina ya mashirika, na waweza kufanya mawasiliano na shirika husika kwa maelezo zaidi ya huduma zao (rejea jedwari lililo nyuma).

Ushauri wa mambo ya ngono na upimaji

Anuani na muda wa usajili wa idara ya Kliniki za usafi wa Afya ya Jamii (kwa wanawake) tazama katika tovuti hii: http://www.dh.gov.hk/english/tele/tele_chc/tele_chc_shcf.html.

Kliniki	Anuani	Muda wa kazi
Kliniki ya Afya ya Jamii ya Chai Wan	West LG5, Specialist Out-patient Department, Pamela Youde Nethersole Eastern Hospital, 3 Lok Man Road, Chai Wan, Hong Kong Simu +852 2595 7500	Jumatano: 2:45 asubuhi-7:00 mchana Jumatatu: 2:30 asubuhi-7:00 mchana Ijumaa: 2:45 asubuhi-7:00 mchana Jumatatu, Jumatano, Ijumaa: 8:00 alasiri hadi 11:30 jioni
Kliniki ya Afya ya Jamii ya Wan Chai (wanawake)	Gorofa ya 7, Tang Chi Ngong Specialist Clinic, 284 Queen's Road East, Wan Chai, Hong Kong Simu +852 3103 2411	Jumatatu: 2:30 asubuhi-7:00 mchana Jumane-Ijumaa: 2:45 asubuhi-7:00 mchana Jumatatu-Ijumaa: 8:00 alasiri-11:30 jioni
Kliniki ya Afya ya Jamii kwa wanawake ya Yaumatei	Gorofa ya 3, Yaumatei Jockey Club Polyclinic, 145 Battery Street, Yau Ma Tei, Kowloon	Jumatatu: 2:30 asubuhi-7:00 mchana Jumane: 2:45 asubuhi-7:00 mchana Jumatano-Ijumaa: 2:45 asubuhi-7:00 mchana

	Simu +852 2388 6634	Jumatatu-Ijumaa:8:00 alasiri-11:30 Jioni Jumanne: 11:30 jioni-2:30 usiku
Kliniki ya Afya ya Jamii ya Yung Fung Shee	Gorofa ya 4, Yung Fung Shee Memorial Centre, 79 Cha Kwo Ling Road, Kwun Tong, Kowloon Simu +852 2727 8315	Jumanne & Alhamisi: 2:45 asubuhi-7:00 mchana Jumanne & Alhamisi: 8:00 alasiri-11:30 jioni
Kliniki ya Afya ya Jamii ya Tuen Mun	Gorofa 5, Tuen Mun Eye Centre, 4 Tuen Lee Street, Tuen Mun, New Territories Simu +852 2459 2958	Jumatatu: 2:30 asubuhi-7:00 mchana Jumatano-Ijumaa: 2:45 asubuhi-7:00 mchana Jumatatu, Jumatano, Ijumaa: 8:00 alasiri hadi 11:30 jioni

Anuani na muda wa usajili **idara ya Kliniki za usafi wa Afya ya Jamii** (kwa wanaume) tazama katika tovuti hii: http://www.dh.gov.hk/english/tele/tele_chc/tele_chc_shcf.html.

Kliniki	Anwani	Muda wa kazi
Kliniki ya Afya ya Jamii ya Chai Wan	West LG5, Specialist Out-patient Department, Pamela Youde Nethersole Eastern Hospital, 3 Lok Man Road, Chai Wan, Hong Kong Simu +852 2595 7500	Jumanne na Alhamisi: 2:45 asubuhi-7:00 mchana 8:00 alasiri-11:30 jioni Jumatatu 2:30 asubuhi-7:00 mchana Ijumaa: 2:45 asubuhi-7:00 mchana
Kliniki ya Afya ya Jamii ya Wan Chai (wanaume)	Gorofa ya 6, Tang Chi Ngong Specialist Clinic, 284 Queen's Road East, Wan Chai, Hong Kong Simu +852 3103 2400	Jumatatu: 2:30 asubuhi-7:00 mchana Jumanne-Ijumaa: 2:45 asubuhi -7:00 mchana Jumatatu- Jumatano & Ijumaa: 8:00 alasiri-11:30 jioni Alhamisi (kwa magonjwa ya ngozi pekee) 8:00 alasiri-11:30 jioni
Kliniki ya Afya ya Jamii kwa wanaume ya Yaumatei	Gorofa ya 5, Yaumatei Jockey Club Polyclinic, 145 Battery Street, Yau Ma Tei, Kowloon Simu +852 2359 4377	Jumatatu: 2:30 asubuhi-7:00mchana Jumatano-Ijumaa: 2:45 asubuhi-7:00 mchana Jumatatu-Ijumaa: 8:00 alasiri-11:30 jioni Jumanne (kwa matatizo yaliyoripotiwa zamani tu): 11:30 jioni-2:30 usiku Jumanne: 2:45 asubuhi-7:00 mchana
Kliniki ya Afya ya Jamii ya Yung Fung Shee	Gorofa ya 4, Yung Fung Shee Memorial Centre, 79 barabara ya Cha Kwo Ling, Kwun Tong, Kowloon Simu +852 2727 8315	Jumatatu: 2:30 asubuhi-7:00 mchana Jumatano & Ijumaa: 2:45 asubuhi-7:00 mchana Jumatatu, Jumatano & Ijumaa: 8:00 alasiri-11:30 jioni
Kliniki ya Afya ya Jamii ya Tuen Mun	Gorofa ya 5, Tuen Mun Eye Centre, 4 mtaa wa Tuen Lee, Tuen Mun, New Territories Simu +852 2459 2958	Jumanne & Alhamisi: 2:45 asubuhi-7:00 mchana Jumanne & Alhamisi: 8:00 alasiri-11:30 jioni

Mashirika yanayo wasaidia watu wanao omba hifadhi, wakimbizi na wadai chini ya mkataba wa mateso wenye nyaraka zinazotambulika kisheria

- Shirika la kutoa msaada wa haraka (AIDS Hotline) lililoko kwenye Idara ya Afya
- Shirika la Rainbow - Hong Kong
- Shirika la shughuli za misaada (AIDS Concern)
- Shirika linalo husika na uwezeshaji wa afya ya jamii (Community Health Organisation for Intervention, Care and Empowerment Limited)
- Shirika la msaada la Hong Kong (Hong Kong AIDS Foundation)
- Kituo cha elimu ya maambukizi ya ukimwi cha kanisa la Mtakatifu John (St Johns Cathedral HIV Education Centre)

Mashirika maalumu yanayowasaidia wafanyabiashra ya ngono

- Shirika la Zi Teng
- Shirika la Action for Reach Out
- Shirika la Midnight Blue

Taarifa juu ya utoaji mimba, mimba, na uzazi wa mpango

- Chaguo la mama (Mother's Choice)

- Shirika la uzazi wa mpango la Hong Kong

Sehemu ya IV

Haki ya kurejeshwa makwao wafanyabiashara ya ngono

Haki katika suala la kuwarejesha makwao

- 1 Kuondolewa kwa watu
- 2 Mtu anaweza kukataliwa kuingia nchini na/au kurejeshwa makwao endapo:
- 3 Amefika Hong Kong au yuko Hong Kong na kwamba ameshindwa kuonesha vitambulisho au hati halali za kusafiria.
- 4 Ameonekana kuwa mhamiaji asiye sitahili ambaye alikuwa haishi Hong Kong kwa miaka mitatu au zaidi.
- 5 Licha ya kuwa mkaazi kwa miaka mitatu, mtu akiingia Hong Kong kinyume cha sheria na alikuwa anakikiuka au alikuwa amekiuka mashariti ya kuishi.

Kumbuka kuwa wakimbi, wanaotafuta hifadhi, na wadai chini ya mkataba wa mateso (CAT) wanaowasilii Hong Kong hawawezi kuondolewa au kufukuzwa au kurejeshwa makwao.

Mamlaka ya kumfukuza mtu nchini

Ufukuzwaji unaweza kuamriwa kama mtu atapatikana na hatia hapa Hong Kong kwa kosa liwezalo pelekea kifungo cha zaidi ya miaka 2 au vyovyote vile gavana atakavyoona inafaa kwa manufaa ya jamii.

Rufaa

Taarifa ya maandishi itatolewa kwa mtu anayeondolewa/fukuzwa na kwamba rufaa yeyote ya kupinga hilo lazima iwasilishwe kwa maandishi ndani ya masaa 24 tangu kupewa taarifa ya kuondolewa.

Anuani za Balozi za Nchi Mbalimbali

Africa

Ubalози Mkuu	Balozi Mkuu	Simu namba	Barua pepe
Angola	Dr. Cupertino De Jesus Pio Do Amaral Gourgel	3798 3888	reception@consuladogeral-Angola.hk
Misri	Mohamed Fahmy	2827 0668	consulate.hongkong@mfa.gov.eg
Nigeria	David Oladipo Obasa	2827 8813	nigeriaconhk@yahoo.com
Africa Kusini	Ms. N. Tambo	2577 3279	sacghgk@netvigator.com
Zimbabwe	Paul Chikawa	2598 0678, 2598 0444	zcghk@biznetvigator.com
<u>Ubalози</u>	<u>Balozi</u>	<u>Simu namba</u>	<u>Barua pepe</u>
Botswana	Alan Nam Cheung-wing	2366 9978	Haihusiki
Burundi	Clifford Lau	5177 2236	cliffordlau@live.com
Cameroon	Dominique Etienne Vessigault	2525 2005	info@camerooncchk.com
Congo	Patrick S.F. To	2793 1313	shufaito@mft.com.hk
Ivory Coast	Andrew C C Ma	2815 9988	amdfkcpa@netvigator.com
Djibouti	Ms. Kathy Chiu Kam-hing, JP	2537 9981	kathychiu@prime-investments.com.hk
Equatorial Guinea	Dr. Vicwood K.T. Chong, JP	2543 1943	Haihusiki
Eritrea	James Huang	2722 1573	Haihusiki
Ethiopia	Dennis Ng Wang-pun, MH	2363 0200	ethiopia_consulate@yahoo.com.hk
Gabon	C.S. Gooljarry	2851 0361	cassam_gooljarry@sino-oceans.com
Ghana	Jonas Wu Fan Ling	2530 3448	ghana@ghana.org.hk
Kenya	Dr. Tam Wing-kun, BBS, JP	2520 5000	wktam@kenyaconsulate.org.hk
Lesotho	Ms. Gloria Ko Lee	2526 3287	consul@lesotho.org.hk
Madagascar	Dr. Hui Chi-ming, GBS, JP	2587 8223	carol@hkaii.org
Mali	Jason Wong Chun-tat	2109 8111	mdoffice@hongthai.com

America

Ubalози Mkuu	Balozi Mkuu	Simu namba	Barua pepe
Argentina	Alfredo Mario Rescic	2523 3208,	consarhk@netvigator.com

		2523 3251, 2523 3274	
Brazil	Antonio José Rezende de Castro	2525 7004	consulate@brazil.org.hk
Canada	Ms. Doreen Steidle	2847 7420	hkng@international.gc.ca
Chile	Mario Ignacio Artaza	2827 1826, 2827 1748	cgchile@netvigator.com
Colombia	Vacant	2545 8547	info@consuladocolombiahk.com
Mexico	Vacant	2511 3305	consulmex@mexico.com.hk
Peru	Mr. David Málaga	2868 2622	peruhkmc@netvigator.com
Marekeni	Stephen M. Young	2523 9011	Haihusiki
Venezuela	Vacant	2730 8099	consulve@biznetvigator.com
Ubalozi	Balozi	Simu namba	Barua pepe
Bahamas	Dr. John Edward Wenham Meredith	2619 6421	Haihusiki
Barbados	Victor T.K. Li	2128 8888	Haihusiki
Cuba	David W.C. Tang	2525 6320	Haihusiki
Grenada	Dr. Johnny S. H. Hon	3656 2838	info@grenada-hk.org
Jamaica	Ms. Evelyn Lu	3552 8538	jamconsulate@yahoo.com.hk
Suriname	Lok Ho-ting	2573 3862	suriname@netvigator.com
Trinidad & Tobago	Dr. Richard S.C. Yapp	2834 4988, 2833 9091	Haihusiki
Uruguay	Dr. Anabella Levin-Freris	2168 0832	afreris@pacific.net.hk urulinks@hotmail.com

Asia

Ubalozi Mkuu	Balozi Mkuu	Simu namba	Barua pepe
Bangladesh	Ashud Ahmed	2827 4278/9	bangladdt@netvigator.com
Brunei Darussalam	Kader Razali	2522 3795	Haihusiki
Cambodia	Luy David	2546 0718	cacghk@netvigator.com
Jamuhuri ya Kidemokrasia ya watu wa Korea	Kim Ik Song	2803 4447	dprkorea@netvigator.com
India	Gaddam Dharmendra	3970 9911, 3970 9900	cg.hongkong@mea.gov.in
Indonesia	Teguh Wardoyo	3651 0200	kjihkg@netvigator.com
Iran	M. A. Tabatabaei Hasan	2845 8003	irancg@iranconsulate.org.hk
Israel	Amikam Levy	2821 7500	info@hongkong.mfa.gov.il
Japan	Yuji Kumamaru	2522 1184	Haihusiki
Kazakhstan	Nurzhan Abdymomunov	2548 3841	office@consul-kazakhstan.org.hk
Korea	Jun Ok-hyun	2529 4141	info@korea.org.hk
Kuwait	Bader S. Al-Tunaib	2832 7866	kuconshk@netvigator.com
Laos	Vacant	2544 1186	lao01_cons@ctimail.com
Malaysia	Jilid Bin Kuminding	2821 0801	malhkong@kln.gov.my
Myanmar	U Wai Lwin Than	2845 0810, 2845 0811	myancghk@biznetvigator.com
Nepal	Binod Kumar Upadhyay	2369 7813	cgnhk@biznetvigator.com
Pakistan	Dr. Ahmad Balal	2827 1966	parephk@netvigator.com
Philippines	Claro S. Cristobal	2823 8501	hongkongpc@philcongen-hk.com
Saudi Arabia	Hammad G. M. Al Rowaily	2520 3200	consulgeneral@saudiconsulate.org.hk
Singapore	Dr. Ker Sin Tze	2527 2212	singcg_hkg@sgmfa.gov.sg
Thailand	Vacant	2521 6481-5	thaicghk@thai-consulate.org.hk
Uturuki	Mehmet Raif Karaca	2572 1331	consulate.hongkong@mfa.gov.tr
Falme za Kiarabu (emirates)	Saeed Hamad Ali Al Junaibi	2866 1823	cg@uae.hk
Vietnam	Pham Cao Phong	2591 4510, 2591 4517	tlsqhk@mofa.gov.vn
Ubalozi	Balozi	Simu namba	Barua pepe
Bahrain	Dr. Chow Yei Ching, GBS	3171 1199	info@bahrainconsulate.org.hk
Cyprus	Kenneth Ting Woo-shou, SBS, JP	2798 1565	Haihusiki
Jordan	David T.C. Lie, SBS, JP	2524 0085	Haihusiki
Maldives	Bob N.Harilela, JP	2376 2114	Haihusiki
Oman	Louis K.C. Wong, JP	2873 0888	fidcr@netvigator.com
Sri Lanka	Dr. Thomas H.C. Cheung, MH	2876 0828	thomascheung@pacificgroup.com.hk

Yemen	Aaron Shum Wan-lung	2334 8612	yemen.consulate@aaronshum.com
-------	---------------------	-----------	--

Ulaya

Ubalози Mkuu	Balozi Mkuu	Simu namba	Barua pepe
Austria	Gerhard Alois Maynhardt	2522 8086	hongkong-gk@bmeia.gv.at
Ubeligiji	Michel Malherbe	2524 3111	hongkong@diplobel.fed.be
Jamhuri ya watu wa Czech	Jaroslav Kantůrek	2802 2212	hongkong@embassy.mzv.cz
Denmark	Torben A. Gettermann	2827 8101 Ext. 122	hkggkl@um.dk
Finland	Ms. Annikki Arponen	2525 5385	sanomat.hng@formin.fi
Ufaransa	Arnaud Barthélémy	3752 9912	Press@consulfrance-hongkong.org
Ujerumani	Werner Lauk	2105 8711	info@hong.diplo.de
Ugiriki	Mrs. Constantina Koliou	2774 1682	grgencon.cg@mfa.gr
Italia	Ms. Alessandra Schiavo	2522 7835	consolato.hongkong@esteri.it
Uholanzi	Robert Schuddeboom	2522 5127 Ext.: 206	information@netherlands-cg.org.hk
Poland	Przemyslaw M. Jenke	2840 0779, 2840 0814	kgrphk@netvigator.com
Ureno	Manuel Carvalho	(853) 2835 6660-2	mail@macau.dgaccp.pt
Romania	Sorin Vasile	2523 3813	hkm@romcongen.com.hk
Urusi	Sergey N. Gritsay	2877 7188	russia@hknet.com
Hispania	Vacant	2525 3041/2	espcgkh@netvigator.com
Sweden	Lars Danielsson	2521 1212	generalkonsulat.hongkong@foreign.ministry.se
Uswisi	Mrs. Rita Hämmerli-Weschke	2522 7147/8	hon.vertretung@eda.admin.ch
Uingereza	Andrew Seaton	2901 3000	information@bcg.org.hk
Ubalози	Balozi	Simu namba	Barua pepe
Albania	Dr. Kennedy Wong Ying-ho, BBS, JP	2867 1362	albania.consulate@gmail.com
Croatia	Sir Gordon Wu Ying-sheung, GBS	2528 4975	gordonwu@hhlmail.com
Estonia	Matthew Lam Kin-hong, MH	2868 3110	info@estoniaconsulate.com.hk
Hungary	Dr. Paul Kan Man-lok, SBS, JP	2878 7555	consulate@hungary.hk
Iceland	Robert Grool	2876 8888	Haihusiki
Ireland	Harry Eugene O'Neill	2527 4897	info@consulateofireland.hk
Latvia	Roger King	2877 5638	Haihusiki
Lithuania	Raj Sital Motwani, BBS, JP	2522 2908	rajsital@netvigator.com
Luxembourg	Leo Kung Lin-cheng, JP	2877 1018	conluxhk@netvigator.com
Malta	Mrs. Vivien Chou Chen	2739 2611	synflex@hkstar.com
Monaco	Tung Chee-chen, SBS, JP	2893 0669	tungcc@oocl.com
Norway	Liu Cheng-Chan	2546 9881	norwayhk@ncchk.org.hk
San Marino	Francis Robert Mullens	2526 2011	SUNRAY33@GMAIL.COM
Jamhuri ya Kislovakia	Willy Lin Sun-mo, SBS, JP	2484 4568	slovakconsulatehk@milos.com.hk
Slovenia	Bernard C.W. Lau	2545 2107	phlandpt@biznetvigator.com

Visiwa vya Oceanic na Pasifiki

Ubalози Mkuu	Balozi Mkuu	Simu namba	Barua pepe
Australia	Les Luck	2827 8881	enquiries.hongkong@dfat.gov.au
New Zealand	Ms. Adele Bryant	2525 5044	nzcghkg@biznetvigator.com
Ubalози	Balozi	Simu namba	Barua pepe
Fiji	Desmond Y.T. Lee	2375 1618	info@fiji-worldchallenge.com.hk
Papua New Guinea	Jim K.C. Or	2499 3611	Haihusiki
Tonga	George Chen	2522 1321	ttohk@hkstar.com
Vanuatu	Cheng Tung-leong	2723 2188	vhkconsulate@yahoo.com.hk

Sehemu ya V

Watoa misaada ya ustawi wa jamii ili kukidhi mahitaji ya kujikimu

Idara ya Ustawi wa Jamii (SWD)

- Mfuko maalumu wa msaada wa hifadhi ya jamii (CSSA) hutoa fedha kwa ajili ya kuinua kipato cha kaya hadi kiwango kinachostahili ili kukidhi mahitaji ya msingi. Hii ni njia ya majaribio na inategemea kama mwombaji ni mkazi wa Hong Kong kwa angalau miaka 7 na kaendelea kuishi Hong Kong mfululizo kwa angalau mwaka 1 kabla ya tarehe ya kufanya maombi hayo. Katika hali ya kipekee, CSSA inaweza kuwa na maamuzi, kwa kibali cha Mkurugenzi wa Idara ya Ustawi wa Jamii, kwa mtu ambaye hawezi kukidhi mahitaji ya makazi. Misaada maalumu kwa waombaji wanao stahili hujumuisha kodi, ada ya shule, gharama muhimu za usafiri, na ukarabati wa vifaa vya matibabu. Maombi ni budi yapelekwe kwenye kitengo cha hifadhi ya jamii kwa njia ya simu, faksi (nukushi), barua pepe, njia ya posta au peleka mwenyewe kwa mkono. Maombi pia yanaweza kufanywa kupitia rufaa kutoka moja ya idara nyingine ya serikali au shirika lisilo la kiserikali.
- Familia na Ustawi wa Mtoto kwenye idara ya ustawi wa jamii (SWD) hutoa aina mbalimbali za ustawi wa mtoto, hii ikiwa ni pamoja na vituo vya kutoa huduma unganishi ya familia (IFSC'S)/vituo vya huduma unganishi.
- Huduma ya matibabu kwa jamii kwenye idara ya ustawi wa jamii (SWD) huendesha vituo 33 vya kutoa huduma ya matibabu kwa jamii kwenye hospitali za umma, katika kliniki za mtaalam maalum (specialist clinic) na kwenye kliniki za tiba za kawaida. Watu ambao hawapati huduma za mfuko wa CSSA wanaweza kuomba msamaha wa kulipia matibabu kupitia kitengo cha huduma ya matibabu kwa jamii – idara ya ustawi wa jamii (hii ni pamoja na waomba hifadhi, wakimbizi na wadai chini ya mkataba wa mateso CAT wenye nyaraka zinazo tambulika).
- Shirika linaloshughukia wakimbizi wanawake (Bethune House Migrant Women's Refuge Ltd).
- Shirika la kimatatafa la huduma za kijamii la Hong Kong (ISS-HK) hutoa msaada kwa wanao tafuta hifadhi na wadai chini ya mkataba wa mateso (CAT) kufuatia rufaa kutoka shirika linalohusiana na familia na ustawi wa motto-idara ya ustawi wa jamii (SWD). Misaada hiyo ni pamoja na chakula; malazi (kukodisha ghorofa lenye uwezo wa kuchukua watu 11 katika ghorofa moja au kutoa kiasi cha kama \$ 1000 kwa ajiliya pango la nyumba); fedha kwa kwa ajili ya gharama za usafiri ili kuhudhulia mahojiano yanayo husana na kuomba hifadhi, au madai chini ya mkataba wa mateso CAT, au maombi ya ukimbizi na kwa ajili ya kupangiwa matibabu; vyoo pamoja na mavazi.
- Jumba la Chungking la matendo ya kikristo (Christian Action, Chungking Mansions Service Centre).
- Shirika la maono kwanza (Vision First).

Makazi ya Umma

- Makazi ya umma ya kutosha na kwa bei nafuu yanapatikana kwa watu wenye uhalali wa kuishi Hong Kong kupitia mamlaka ya makazi ya Hong Kong (HKHA) na shirika la makazi la Hong Kong (HKHS).
- Huduma ya makazi kwa wanawake walionyanyaswa (idara ya ustawi wa jamii) hutolewa katika vituo 5 vya wakimbizi ambavyo hutoa makazi ya muda mfupi kwa wanawake na watoto wanao kabiliwa na migogoro na uhasama katika familia zao:
 - Makazi ya Wai On (kwa wanawake), simu +852 2793 0223
 - Makazi ya Harmony House, simu +852 2522 0434
 - Makazi ya Serene court (Mahakama ya Serene), simu +852 2787 6865
 - Makazi ya Sunrise court (Mahakama ya mawio ya jua), simu+852 2890 8330
 - Makazi ya Dawn court (Mahakama ya mapambazuko), simu +852 2243 321

Sehemu ya VI

Msaada wa kisheria na huduma za tafsiri

Huduma za msaada wa kisheria

Idara ya Msaada wa Sheria inatoa uwakilishi wa kisheria na wakili kwa waombaji wanaostahili, na kama ni lazima, wakili mkuu katika kesi za madai au jinai kwa kuwasiliana na huduma za msaada wa kisheria kupitia simu namba 2537 7677 au kupitia tovuti hii <http://www.lad.gov.hk/eng/wnew/event.html>.

Waombaji kwenye UNHCR au wadai chini ya mkataba wa mateso (CAT) hawana uwakilishi wa kisheria wa kujitegemea unaofadhiliwa na masharti ya serikali ya msaada wa kisheria na hutegemea zaidi wanasheria wenye kutoa msaada wa kisheria wa kujitegemea au fedha binafsi.

Mashirika yanayo saidia wakimbizi, waomba hifadhi, na wadai chini ya mkataba wa mateso (CAT) wenye hati zinazo tambulika kisheria ni haya yafuatayo:

- Pathfinders
- HKRAC
- St John's Cathedral – Helpers for Domestic Helpers
- Christian Action
- Bethune House Migrant Women's Refuge

Mashirika yanayotoa msaada kwa wafanyakazi wa ngono ni haya yafuatayo:

- Action for Reach Out
- Midnight Blue
- Zi Teng

Huduma za tafsiri

- Huduma ya ukalimani (tafsiri) hutolewa na serikali, lakini siyo rahisi kupatikana kwa makabila madogo madogo.
- *Shirika la CHEER hutoa huduma za tafsiri zifuatazo :*
 - Huduma ya tafsiri ya simu (TELIS). Wakalimani/wafasili hutoa huduma za kutafasiri simu kutoka lugha ya kiingereza kwenda kwenye lugha nyingine 7 (Bahasa Indonesia, Tagalog, Thai, Kihindu, Nepali, Punjabi, Urdu) na kinyume chake na pia wakati rasmi wa kukutana unaweza kuandaliwa kwa ukalimani unaochukuwa kipindi kirefu.

Huduma ya tafsiri ya ana kwa ana (OSIS). Mfanyakazi hutoa maelezo ya mdomo ya moja kwa moja juu ya maana ya makala husika kutoa katika lugha ya kiingereza kwenda lugha 7 zinginezo.

- *Shirika la Christian Action, la huduma ya makabila madogo madogo (ethnic minorities).*

Sehemu ya VII

Haki za kieleimu

Mfumo wa elimu

- Watoto wote wanaostahili wanahaki ya kupata elimu bure kwa miaka 9 (bila kujali kama wanaongea kichina) na wazazi wenye haki ya makazi katika Hong Kong wanalazimika kuwapeleka watoto wa kati ya miaka 6 hadi 15 shuleni kwa kutumia huduma ya msaada inayotolewa kwa watoto waliofika kwa mara ya kwanza wasio ongea kichina kwa ajili ya kuwawezesha kuzoea mfumo wa asili wa elimu uliopo. Ofisi ya elimu imeandaa taarifa na kutoa makablasha ya taarifa kwa wazazi kwa lugha za Kiingereza, Kichina, Kibahasa Indonesia, Kihindi, Kinepali, Kitagalog, Kithai na Kiurdu ambazo zaweza kupatikana kwenye tovuti hii: <http://www.edb.gov.hk/index.aspx?nodeID=4211&langno=1>.
 - Taarifa juu ya elimu na huduma zake mbalimbali zinaweza kupatika pia kaika tovuti hii: www.edb.gov.hk/ncs, www.edb.gov.hk/nac-e na huduma ya maulizo kwa njia ya simu ya moja kwa moja kwa masaa 24 hupatikana kwa simu namba (+852 2891-0088).
 - Hakuna sera ya wazi au mwongozo unaohusiana na haki za elimu kwa watoto wa wakimbizi, waomba hifadhi, na wadai chini ya mkataba wa mateso (CAT). Lakini, ilikufaidika na huduma bure ya elimu ya miaka 9, watoto lazima wawewameandikishwa kwenye idara ya uhamiaji (kwa mfano katika gazeti la serilakali linalotambulika) na stahiki yao

kuthibitishwa na Mkurugenzi wa idara ya uhamiaji ambaye anashughulikia maombi mbalimbali.

- Shirika la ISS-HK litajadili ya watoto kama litaamini yatakuwa ni kwa faida wanaotafuta hifadhi na/au wadai chini ya mkataba wa mateso (CAT).
- Shirika la Vision First.
- Shirika la Christian Action, Chungking Mansions Service Centre hutoa msaada wa elimu na usafiri kwenda shuleni. 0687337547.

Ufundi na mafunzo ya lugha

Kunamipango mbalimbali ya mafunzo ya ufundi na lugha kwa ajili ya wahamiaji halali. Tazama katika tovuti hii: www.gov.hk/en/residents/education/continuing/

- Baraza la mafunzo ya ufundi (Vocational Training Council)
- Shirika la matendo ya Kikristo (Christian Action)
 - o Kituo cha SHINE kwa ajili ya makabila madogo (SHINE Centre for Ethnic Minorities)
 - o Kituo cha Chungking Mansions (Chungking Mansions Service Centre)
 - o Mpango wa wafanyakazi wa majumbani (Domestic Worker Programme)
 - o Kituo cha Mafunzo (Training Centre)
- Shirika la Caritas - Education Services Division
- Shirika la Hong Kong Christian Service
- Shirika la Huduma za Jamii za Kimataifa (ISS-HK) tawi la Hong Kong
 - o HOPE Support Services for Ethnic Minorities
- Shirika la huduma za Kikristo la Hong Kong
 - o Centre for Harmony and Enhancement of Ethnic Minority Residents (CHEER) hutoa mafunzo ya lugha (Kiingereza na Ki-Cantonese kwa wasomaji wa kiwango cha chini, kati na juu).
 - o Kituo cha mafunzo cha Kwun Tong (Kwun Tong Vocational Training Centre) hutoa programu mbalimbali za mafunzo ya ufundi stadi kwa watu wasiobahatika maishani kijamii na kielemu katika Hong Kong.
- Shirika la St John's Cathedral.
- Shirika la Vision First.
- Shirika la Midnight Blue.
- Shirika la Zi Teng.

Sehemu ya VIII

Majukumu ya kisheria ya waajiri wa wafanyakazi wa ngono

Wahamiaji haramu ikiwa ni pamoja na wakimbizi, waomba hifadhi na wadai chini ya mkataba wa mateso (CAT) hawaruhusiwa kufanyakazi katika Hong Kong na wanaweza kukabiliwa na faini ya hadi HK\$350,000 na kifungo cha miaka 3.

Wahamiaji kisheria wanaoshiriki biashara ya ngono wanaruhusiwa kufanyakazi kama wafanyakazi waliojajiri katika biashara ya ngono. Mtu yeyote akipatikana akimuajiri mtu mwingine kama mfanyakazi wa ngono atakabiliwa na kifungo cha hadi miaka 14.

Wahamiaji kisheria kushiriki kazi ya kisheria (klabu za usiku, majumba ya maseji, baa za vileo) wanastahili kupata ulinzi wa ajira kama wanavyostahili wafanyakazi wa Hong Kong, na kwamba wanatakiwa kulipa kodi kwa mujibu wa sheria ya ajira na sheria ya vyama vya wafanyakazi.

Sehemu ya IX

Haki za ajira na wajibu wa kodi

Haki za ajira

Wahamiaji halali wanaojishulisha na biashra ya ngono

Wafanyakazi wa ngono

- 1 Hawaruhusiwi kukodisha walinzi au mlinzi.
- 2 Hawaruhusiwi kufanyakazi pamoja ili kuijilinda.
- 3 Hawaruhusiwi kuajiliwa na mtu yeyote na kwamba hawawezi kujadili sheria na masharti ya kazi zao.
- 4 Hawawezi kuunda umoja, ingawa umoja usiorasmi umeanzishwa na Zi Teng.

Mashirika yanayotoa huduma za msaada kwa wafanyabiashara wa ngozo

- Shirika la Zi Teng.
- Shirika la Action for Reach out (AFRO).

Wahamiaji halali wanaojishughulisha na kazi halali (klabu za usiku, majumba ya maseji, baa za vileo) wanastahili kupata ulinzi wa ajira kama wanavyostahili wafanyakazi wa Hong Kong, ikiwa ni pamoja na mshahara wa ulinzi, siku za mapumziko, malipo ya likizo ya kila mwaka, posho ya ugonjwa, uangalizi wa uzazi, malipo ya kupoteza kazi, malipo ya utumishi wa muda mrefu, ulinzi katika ajira, kusitisha mkataba wa ajira, ulinzi dhidi ya kupambana na umoja wa ubaguzi, taaluma ya afya na ulinzi wa usalama, na kulindwa kutokana na ubaguzi kwa misingi ya jinsia, kuo au kutokuolewa, mimba, na unyanyasaji wa kijinsia. Kama mtu yeyote, kinyume cha sheria, akinyimwa fursa sawa katika mambo yaliyo tajwa hapo juu anaweza kufungua malalamiko kwenye kamati ya fursa sawa (EOC) na kuleta kesi za kisheria mbele ya mahakama ya wilaya chini ya sheria ya kupambana na ubaguzi.

Wajibu wa kodi

- Utozwaji kodi wa wafanyabiashara wa ngono ni tatizo lisilowazi kutokana na hadhi ya kazi isiyo kamili na mara nyingi hadhi ya wahamiaji wafanyakazi wa ngono isiyo halali.
- Wahamiaji haramu ambao ni wafanyakazi wa ngono (ikiwa ni pamoja na wanaotafuta hifadhi, wakimbizi, na wadai chini ya mkataba wa mateso – CAT) hawaruhusiwi kufanyakazi Hong Kong na kwahiyo hawana wajibu wa kulipa kodi.
- Wahamiaji halali ambao ni wafanyabiashara ya ngono
 - Wafanyabiashara haramu wa ngono (kama vile kufanyakazi katika madanguro) ni kinyume cha sheria na hivyo hawawajibiki kulipa kodi.
 - Wafanyabiashara wa ngono halali (waliojijiri wenyewe) → eneo la kijivu/haijulikani.
 - Wafanyakazi halali (kama vile kwenye klabu za usiku, majumba ya maseji, baa za vileo) wanawajibu wakulipa kodi, wakati huo huo, huduma ya ziada ya ngono inayotolewa katika mazingira hayo huwekwa katika kipengele I au II.
- Mahala ambapo ushuru unatakiwa kulipwa, mtu anapaswa kulipa kodi kutokana na mapato yatokanayo na kazi husika, na endapo mtu atapokea kodi rejeo kutoka kwenye idara ya mapato ya ndani ni lazima ikamilishwe na kuwasilishwa kabla ya tarehe ya mwisho kwa kumbukumbu.

Mahali ambapo kunawajibu wa kulipa kodi kwa mtu aliyejijiri mwenyewe, mtu atatozwa kodi ya faida wakati mtu huyo anawajibu fulani ikiwa ni pamoja na kuweka kumbukumbu ya biashara, kuandaa hesabu kwa kuzingatia rekodi za uhasibu, kukamilisha na kuwasilisha kodi rejeo kwa kutoa taarifa za faida ya biashra au hasara na malipo ya kodi.

Sehemu ya X
Maelezo ya mawasiliano ya watoa huduma wa msaada

Huduma kwa wafanyabiashara wa ngono

* Huduma zilizopo kwa wahamiaji haramu (Wakimbizi, waomba hifadhi na wadai chini ya mkataba wa mateso) wenye barua za utambulisho

^ Huduma kwa ajili ya makabila madogo

<u>Mtoa huduma</u>	<u>Msaada uliopo</u>	<u>Anwani</u>	<u>Lugha</u>
# Action for Reach Out	<p>Shirika lisilo la kiseikali linalosaidia wanawake wanaofanyakazi katika biahara ya ngono la Hong kong (Non-government charitable organisation assisting women working in sex industry in HK)</p> <p>Huduma zenyewe ni hizi zifuatazo:</p> <ul style="list-style-type: none"> - Msaada wa ushauri wa kisheria - Kuwasindikiza wanawake waendapo kituo cha polisi au kwenye mfumo wa kisheria - Kuwatia moyo na kuwawezesha wanawake kuunda vikundi vya msaada kama vile chombo cha rufaa kwa ajili ya uchunguzi wa afya, ushauri wa kisheria, ushauri nasaha, na kama ni lazima makazi ya muda. - Kutoa taarifa juu ya vipindi vya haki za kisheria, elimu ya afya, ushauri nasaha wa familia na mafunzo ya ujuzi. - Taarifa juu ya maambuzo ya virusi vya UKIMWI na UKIMWI (HIV/AIDS) - Kutoa huduma bure ya upimaji wa magonjwa ya zinaa na magonjwa ya wanawake (STD and gynaecological)siku ya Jumanne kuanzia saa 5.00 asubuhi hadi 6.15 mchana, na kuanzia saa 8.00 mchana hadi 11.00 jioni. 	<p>Anwani: PO Box 98108, TST Post Office, Tsim Sha Tsui, Kowloon</p> <p>Simu: +852 2770 1065</p> <p>Kiungo: 7110 9318 call 394</p> <p>Faksi: +852 2770 1201</p> <p>Simu ya muda wote: +852 2770 1002</p> <p>Barua pepe: contact@afro.org.hk</p> <p>Tovuti: www.afro.org.hk</p>	<p>Cantonese</p> <p>Mandarin (Kichina)</p> <p>Kiingereza</p>
AIDS Concern	<p>Huduma za mashirika yasiyo ya kiserikali (Non-government organisation Services):</p> <ul style="list-style-type: none"> - Ushauri nasaha na upimaji wa hiari (VCT) ni huduma ya mara moja inayotoa ushauri nasaha, upimaji wa virusi vya UKIMWI, na magonjwa ya zinaa (Kaswende, , Klamidia [Chlamydia], na haipatitis B[Hepatitis B]). - Utoaji wa supu kwa watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI na UKIMWI - Huduma ya usafiri wa bure kwa watu wanaoishi na virusi vya ukimwi na ukimwi (PHAs) 	<p>Anwani: 17B, Block F, 3 Lok Man Road, Chai Wan</p> <p>Simu: +852 2898 4411</p> <p>Faksi: +852 2505 1682</p> <p>Kuweka muda wa upimaji virusi vya ukimwi: +852 2394 6677</p> <p>Barua pepe: enquire@aidsconcern.org.hk</p> <p>Tovuti: www.aidsconcern.org.hk</p>	<p>Cantonese</p> <p>Mandarin</p> <p>Kiingereza</p>
^ Asian Migrant Centre	<p>Huduma zitolewazo kwenye kituo cha kujifunzia maarifa:</p> <ul style="list-style-type: none"> - Hutoa huduma za habari, usimamizi, utafiti na uchapishaji - Utetezi na uunganishaji wa kazi kati ya wafanyakazi wahamiaji wa ndani 	<p>Anwani: 13/F, Flat 6, Blk A, Fuk Keung Ind. Bld</p> <p>66 Tong Mei Road, Kowloon</p> <p>Simu: +852 2312 0031</p> <p>Faksi: +852 2992 0111</p>	<p>Tovuti ipo kwa Kiingereza</p>

		Barua pepe: amc@asian-migrants.org Tovuti: www.asian-migrants.org	
^ Asia Pacific Mission for Migrants	Kikuo cha Mkoa/Kikanda kinachosaidia harakati za wahamiaji kwa njia ya utetezi, kupanga na kujenga mahusiano: <ul style="list-style-type: none"> - Kutoa ushauri kwa wafanyakazi waliosongwa na dhiki/mashaka - Kutoa elimu kupitia shule rafiki maalumu - Kutoa msaada wa kisheria kwa kesi za uhamiaji na ajira - Kutoa msaada wa tafsiri kutoa lugha ya Kichina kwenda Kiingereza 	Anwani: c/o Kowloon Union Church No. 2 Jordan Road, Kowloon Simu: +852 2522 8264 Faksi: +852 2723 4559 Barua pepe: apmm@hknet.com Tovuti: www.apmigrants.org	Kiingereza Mandarin Cantonese
* ASTC Programme, ISS-HK	Waomba hifadhi na wakimbizi wanaoweza kustahili msamaha wa matibabu kupitia mpango huu ambao unasaidiwa na idara ya ustawi wa jamii (SWD)	Anwani: 1/F, Li Po Chun Health Centre, 22 Arran Street, Prince Edward, Kowloon Simu: +852 2578 2126 / 2578 2718 Barua pepe: astc@isshk.org	Tovuti iko kwenye Kiingereza
^ Bethune House Migrant Women's Refuge	Huduma zinazotolewa na shirika la hisani lililosajiriwa kwa ajili ya kushughulikia matatizo ya wanawake wahamiaji wenye dhiki/mateso, hususan wafanyakazi wa kazi za ndani (Kwa muavuli wa St John's Cathedral Mission in Action programme for Migrant Workers) Huduma zitolewazo: - Ushauri nasaha na msaada wa kisheria - Shughuli za kijamii - Kwa wakati mwingine misaada ya hali (vitu) na mali - Misada bure na mahali pa kukimbilia (kwa kuzingatia wasaidizi wa ndani) - Kuwasindikiza watu binafsi katika idara za uhamiaji na kazi	Anwani: c/o Kowloon Union Church, 4 Jordan Road, Kowloon Simu: +852 2721 3119 Barua pepe: bhmwr@hknet.com Tovuti: www.migrants.net/_events/Bethune_open_haus.html	Kiingereza, Cantonese
^ Caritas Hong Kong Links of Harmony – Social Services for Ethnic Minorities	Huduma za misaada na ukarabati kwa watu maskini na wenye dhiiki/shida: - Kazi za huduma za jamii - Huduma za kieleimu - Huduma za matibabu - Maendeleo ya jamii - Huduma za elimu na mafunzo	Anwani: 1/F, 256A, Prince Edward Road West, Kowloon Simu: +852 2339 3713 Faksi: +852 2794 3667 Barua pepe: info@caritas.org.hk Tovuti: www.caritas.org.hk	Cantonese Kiingereza

